

# Mradi wa Haki katika Misitu unaendelea kujitana...

Na Eliasi Monga - Meneja mradi Haki katika Misitu

**M**radi wa Haki katika Misitu, mradi wa ubia kati ya shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) umezidi kutanua shughuli zake na sasa unafanya kazi katika kanda za kitaifa sita. Awali mradi huu mwenye lengo la kusisitiza uwajibikali na uboreshwaji wa utawala katika sekta ya misitu nchini ulikuwa unafanya kazi katika kanda tatu ambazo ni kanda ya kaskazini, mashariki na kusini. Kuanzia mwaka huu wa 2012, mradi umeongeza kanda ya nyanya za juu kusini, magharibi na kanda ya kati katika shughuli zake.

Mradi umeshafungua ofisi za kanda na kuajiri waratibu wa kanda;

1. Ofisi ya kanda ya magharibi ipo Kigoma. Mratibu wa Kanda ni Ndugu Benedict Minja. Namba ya simu ni 0786092821
2. Ofisi ya kanda ya Nyanja za juu kusini ipo Iringa mjini eneo la Kisesa. Mratibu wa kanda ni bwana Remmy Nasua. Namba ya simu ni 0786092424
3. Ofisi ya kanda ya kati ipo Babati. Mratibu wa kanda ni bwana John Reuben. Namba ya simu ni 0786093307

Katika kipindi kifupi cha miezi miwili, mradi umeshatekeleza shughuli mbali mbali katika kanda

mpya ikiwa ni pamoja na kuitembelea mitandao yote ya MJUMITA na kutoa mafunzo ya utawala bora kwa wanachama, kutoa mafunzo kwa baadhi ya wanamjumita namna ya kushiriki katika ufuatiliaji wa utawala wa misitu katika vijiji vyao na kutambulisha shughuli mbalimbali ambazo mradi utakuwa ukitekeleza kwa kushirikiana na wanamjumita na wadau wengine.

Pamoja na shughuli za ufatiliaji wa hali ya utawala wa misitu katika vijiji, mradi pia utakuwa ukipokea taarifa za uhalifu katika misitu kutoka kwa wananchi na kuzipeleka kwa mamlaka husika ili kuchukua hatua. Mwananchi yeyote hasa mwana mjumita atatakiwa kutoa taarifa sahihi kupitia namba za simu za kanda na mratibu wa kanda atapeleka taarifa hizo katika mamlaka husika ili kuchukua hatua haraka inavyowezekana. Namba za kanda ni kama zilivyotajwa hapo juu, dhamira ni kuwaunganisha wananchi na mamlaka husika ili kwa pamoja washirikiane kukomesha uhalifu wowote unaotokea katika misitu.

Mradi unapenda kutoa shukurani zake kwa wanamjumita na wadau wengine wote hasa serekali za wilaya na vijiji na mashirika yasiyo ya kiserekali kwa namna ambavyo wameupokea mradi na kutoa ushirikiano wa hali ya juu. Aidha mradi unaomba ushirikiano huo uendeleo.